

JINA.....NAMBA YAKO.....

SAHIHI YA MTAHINIWA.....

TAREHE.....

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA TATU

FASIHI YA KISWAHILI

MUDA: Saa 2½

## MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA SUBUKIA

102/3

FASIHI YA KISWAHILI

KARATASI YA 3

Julai/Agosti, 2013

### MAAGIZO

- ❖ Swali la kwanza ni la lazima
- ❖ Chagua maswali mengine matatu kutoka Yale yaliyobakia
- ❖ Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

### YA WATAHINI PEKEE

SWALI	ALAMA YOTE	ALAMA YA MWANAFUNZI
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
5	20	
6	20	
7	20	
<b>ALAMA JUMLA</b>		

## **SEHEMU YA A: USHAIRI**

*Soma mashairi yafuatayo kasha ujibu maswali yanayofuata.*

### **A Nakukumbuka**

Mi nawe mbali tungawa, na kukumbuka  
Lau ‘ngekuwa nambawa, ningaliruka  
Ni muhali hili kuwa, nasikitika.

Mi nawe mbali tungawa, sitahamili  
Pamoja takuja kuwa, sote wawili  
Mwombe uhai moliwa, na njema hali

### **B Kwa heri**

Nakuaga ndugu yangu, kwa heri ya kuonana  
Naondoka nenda zangu, hiwa na simanzi sana.  
Simanzi moyoni mwangu, kwa tulivyozoweyana  
La kutenda ndilo sina, ela kwenenda nendako

Nawe kaa kwa salama, salama wa salimini  
Nakutakiya uzima, na furaha ya moyoni.  
Siku moja ni lazima, tutakutana mwadani  
Kwa hili nina yakini, bora sote tuwe hai.

Siwati kukukumbuka, popote nitakapokuwa  
Na ingawa naondoka, mimi mbali nawe kuwa  
Daima hutanitoka, ndani ya change kifuwa.  
Hakuna ch akukutowa, nendapo naenda nawe.

## **Maswali**

1. Eleza tofauti baina ya mashairi haya katika nyanja zifuatazo

- a) Muundo (alama 4)
- b) Maudhui (alama 2)
- 2. Onyesha namna mshairi alivyotumia uhuru wa kishairi katika mashairi yote mawili. (alama 4)
- 3. Andika methali mbili zinazoafikiana na mashairi yote mawili. (alama 2)
- 4. Andika ubeti wa pili katika kila shairi kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- 5. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 4)
- a) Sitahimili
- b) Mwandani
- c) Moliwa
- d) Siwati

**SEHEMU YA B: RIWAYA  
UTENGANO**

2. He, shogaangu nimekufuata njia nzima wapi sikukuona. Nikajua unakimbilia pahala hapa”.
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - b) Orodhesha sifa nne za msemewa. (alama 4)
  - c) Ni yapi yaliyofuatia muda mfupi baada ya dondoo hili. (alama 2)
  - d) Eleza changemoto tano zilizomkabili msemewa. (alama 10)
  - 3. Eleza migogoro inayowakabili wahusika wafuatao katika riwaya ya utengano.
    - a) Maksiudi (alama 10)
    - b) Maimuna (alama 10)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA- MSTAHIKI MEYA**

- 1. Jadili matumizi ya mbinu zifuatazo katika tamthilia ya Mstahiki Meya
  - a) Kinaya (alama 10)
  - b) Majazi (alama 10)
- 2. a) Onyesha vile umma unavyopokea huduma mbaya katika Mstahiki Meya. (alama 10)
- c) Onyesha vile wahusika wafuatao wanasawiriwa katika Msathiki Meya.
  - i) Diwani wa tatu

ii) Mhubiri

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

1. “Mimi nilitaka mke. Mwanamke mbichi, nimvumbike mwenyewe mpaka aive.”
  - a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - b) Eleza tamathali za usemi zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4)
  - c) Kwa kurejerea hadithi zozote nne eleza  
“Asili ya ndoa.” (alama 12)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

“Mjukuu wangu, masomo ni jambo muhimu sana. Ufikapo shuleni na kuanza maisha ya shule ya upili, usijingize katika mambo ya dunia- anasa na raha nyingi. Vifanye vitabu rafiki wa karibu. Wasikize waalimu na uzingatie wanayoyasema, saidiana na wenzako na utie bidii za mchwa katika masomo. Kumbuka kuwa elimu ndio ufunguo wa maisha mema hapo usoni.”

**Maswali**

- a) Tambua kipera cha fasihi simulizi kinacho husishwa na kifungu hiki. (alama 2)
- b) Taja sifa za kipera hiki. (alama 8)
- c) Taja umuhimu wa kipera hiki katika jamii. (alama 8)
- d) Matumizi ya kipera hiki huwa na lengo gani katika maisha ya kila siku katika jamii. (alama 2)

**ANSWERS:**

Order a copy of answers from [www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy](http://www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy)

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs